# Kukata Rufani

## Kwa

# MUNGU

**Leo Juu Ya Mateso,
Unayopitia Na Mungu
Akujibu Leo Kwa
Matendo Dhahiri**

*Imetayarishwa Na Mwonaji, Mwl. Na Mtumishi*

**DORINA JOSIAH KABYEMERA**

©2026

*Imetayarishwa Na Mwonaji, Mwl. Na Mtumishi*

**DORINA JOSIAH KABYEMERA**
**Simu: +255 767 810 008**
**+255 714 810 008 +255 683 810 008**
Barua pepe: dorjosiah@gmail.com / dstarconsultant@gmal.com
**S.L.P DAR ES SALAAM, TANZANIA**

ISBN 978-9912-42-129-5

**KIMECHAPWA NA: Excellentone Graphics & Print**
**P.O BOX 72635 UBUNGO, DAR ES SALAAM, TZ.**
**MKURUGENZI: FADHILI JULIUS IBRAHIM**
**SIMU: +255 756 964 536, +255 689 776 860**
**Barua Pepe: *fadhilijuliasi@gmail.com***

**Haki zote zimehifadhiwa:**

Hairuhusiwi kunakili, kuchapisha au kutumia sehemu yo yote ya kitabu hiki kwa namna yoyote ile, kama: kutafsiri, Electronic, maigizo ya Sanaa, kuiga, kunakili, kutoa nakala kivuli, au kutoa baadhi ya maandishi ya kitabu hiki kwa namna yoyote ile; bila idhini ya mwandishishi kwa maandishi.

# YALIYOMO

SHUKRANI..........................................................5
UTANGULIZI.....................................................9

SURA YA 1 ....................................................12
Kukata Rufani Kwa Mungu Leo Juu Ya Mateso, Unayopitia Na Mungu Akujibu Leo Kwa Matendo Dhahiri ..........................................................12

KUKUZULIA UONGO/KUKUSEMEA UONGO14

KUKUCHAFULIA JINA......................................15

KUPEWA NAFASI (CHEO):...............................17

KUKATALIWA:................................................18

KUKOSA MTU WA KUKUINUA AU KUKUSHIKA MKONO .......................................26

KUKUBALIKA: ................................................27

KUTENGENEZEZEWA MAGONJWA....................28

KIRI NA USEME HIVI: ........................................38

KUHUSU MWANDISHI.......................................41

# SHUKRANI

Kwa uchache kama si kwa wingi kwanza namshukuru Mungu sana kwa kunipendelea kunipa uhai kuandika kitabu hiki leo hii kama Mwonaji, Mwl na Mtumishi ambaye nimejikita katika kuongea na watu kwa kuwatia moyo (Motivation Speaker au Consultation).

Upendeleo huu wa Mungu hasa kuandika kitabu hiki, ikiwa ni zawadi kubwa ya kufuta sehemu ya machozi na kupoza kiu ya uandishi ili kuonyesha talanta niliokuwa nao tangu nikiwa mdogo na sasa KITABU hiki kiko mkononi mwa msomaji.

Ikiwa ni ombi langu kwa Mungu lenye ushindi hakika kulitimiza kusudi langu kwa mapenzi yake, ili niweze kuandika vitabu vingine kwa mapenzi yake kila wakati Mungu anaporuhusu; Ili kuachilia neno la hekima na maarifa, kwa njia ya uandishi wa neno la kutia moyo na uponyaji **(The Joy of Salvation and The Power of Healing).**

Naishukuru familia yetu hususani mama Zuhura Kabyemera Kemibaro ambaye ni Marehemu kwasasa, kwa malezi mazuri sana na Upendo kwetu usiokuwa wa kifani, bila kumsahau baba Josiah Kabyemera ambaye ni marehemu, kwasasa aliyetufundisha kwa maneno machache (pointi).

Ninawashukuru dada zangu kwa upendo bila kusahau kaka zangu maana hawa wote mamehusika kunilea kama mdogo wao wa mwisho kimwili na kiroho kwa kimaadili na makuzi mema.

Zaidi namshukuru sana Mungu kwa kunipa mme mzuri wa ndoa mpendwa ambaye nimempenda kwa moyo wangu wote, na kumheshimu akanioa kwa ndoa ya Kikiristo Paul M. Steven kupitia Baraka za wazazi na familia zote mbili kuungana kwenye maombi mpaka Kuolewa nchini Uganda mji wa Fort Portal.

Lakini kitabu hiki kina toka sasa, nikiwa na ndoto ya kuandika vitabu vingi; Na kuweka vitu kwenye matendo ikiwa ni pamoja na ofisi yangu ya D'STAR STATIONERY & CONSULTANT ambayo Mungu mwenyezi ameibariki kuipa Baraka ya madhabahu ya KUONA, KUOMBA na

KUFUNDISHA. Na sasa kuibua UANDISHI wa VITABU na kuandika neno la Mungu kila siku.

Ninawashukuru wazazi wangu wa kiroho wote tangu nimezaliwa mpaka sasa, kwani ni wengi, na sasa uandishi huu ninawataja wachache kwa malezi yao mema; Kwa kuwataja kwanza ni mlezi wa sasa Mch. Manase Lema (Mtaa wa Mapinga, Bagamoyo Pwani).

Prof. na Mch Faith K. Lugazia (mlezi kwaya ya Talumbeta wamama DMP), Bila kumsahau Askofu Bagonza (Kutoka Dayosisi mama ninakozaliwa karagwe), Mch. Enoki Thobias Bwege (Mlezi wa ndoa yangu, binamu & mshenga,).

Mch. Chars Mzinga (chaplain Azania Front), Mch. Elias Lugome (Ubungo Kibangu), Mch Raymond Joram Mandu –kutoka Shinyanga hawa wote ni kutoka KKKT, Pastor Makuma Titus Shem (toka Uganda).

Na bila kuwasahau watumishi mbali mbali walionitia moyo kwa maombi ya kusema nami kwa Neno la Mungu wakisema songa mbele na kazi ya

Mungu, na yeye yuko pamoja nawe mwezeshaji ni Mungu.

Ninamshukuru Mrs Jane Amani Mangowi (Regional Academic Officer (RAO-DODOMA) ambaye amenitia moyo kwa kusema kazi ya Mungu isonge mbele; Pia Mungu awabariki watu wote hata kama sijawataja kwa majina yao, ila natambua mchango wenu mbele za Mungu atawalipa sawa sawa na mapenzi yake.

# UTANGULIZI

***Kwa maana mioyo ya watu hawa imepumbaa, na masikio yao ni mazito ya kusikia, Na macho yao wameyafumba, Wasije wakaona kwa macho yao. Na kusikia kwa masikio yao, Na kufahamu kwa mioyo yao, Na kubadili nia zao nikawaponye."***

**Matendo ya Mitume 28:27**

KUKATA RUFANI si kitu kidogo, kwani kukaa na kuandika kitabu hiki, ni baada ya kuona mambo mengi kwenye jamii.

Imekuwa kawaida kwenye jamii kuyachukulia kawaida (poa) nikimaanisha matokeo baada ya tatizo, haya fuatiliwi na huleta magonjwa na vifo vya ghafla; Hadi wengine kuuwawa baada ya kupungua kwa amani kwenye jamii, ikiwa ni pamoja na ndoa kuvunjika, kufukuzwa kazi kutokana na familia kutofautiana imani, Ukabila, ubinafsi na tamaa ya pesa kuliko utu.

Hali ya kuwajibika imepungua kwenye jamii, kwa kuzingatia utandawazi kuongezeka na kusahau

kufanya kazi (kuzalisha) kwa kiwango. Ili mtu husika alishe familia yake (baba au mama), hata kusomesha watoto na kuwapatia mahitaji muhimu. Kutojiandaa na kuandaliwa kwa vijana wakiwa wadogo wakati wa makuzi wakiwa na wazazi au walezi, na nyumbani au mashuleni kunapelekea kuibua kiburi kutawala kwenye vichwa vya watu baadae, ambapo hupelekea kuathirika, kuwa na dharau ya mke au mme kujenga tabia dharau, kutoheshimiana baadae.

Na hii inatokana na mtu mmoja kukosa malezi bora ambaapo hupelekea mtu mzima kutoshaurika na wazazi, walezi ama washauri (counselor) akiwa mtu mzima. Na uko usemi unaosema “SAMAKI MKUNJE ANGALI MBICHI” maana yake, neno la hekima na maarifa hukosa wakati husika kwa mtu sahihi ili apate baraka.

Kitabu hiki nimekiandika kwa kumuomba Mungu sana, ili kuamsha hisia na hamasa za wasomaji ambao ni wazazi juu ya kusisitiza madili ya kiroho, malezi, makuzi ya vijana yatiliwe mkazo.

Maana kutofuatilia mtoto kwa karibu nyumbani, shuleni, hata anapokuwa peke yake, hupelekea

kuleta madhara ya upweke, kujikataa na kujitenga ambayo inachangia tabia zinazokua kwa uficho, na kuharibu mwenendo wa kijana, hadi anapofikia ngazi ya utu uzima.

Kitabu kinalenga zaiidi na kutilia mkazo watu kuzingatia neno la Mungu huku wakisubiri kwa kuacha "***WIVU WA KIMIUNGU***" ambao hupelekea maafa kwenye jamii ikiwepo, vifo na kuharibika kiakili, yaani msongo wa mawazo ***(afya ya akili)*** inayoleta watu kupoteza utu na mwelekeo wa maisha. Kitabu hiki ni hazina ya kuboresha maisha ya mtu binafsi, kuanzia nyumbani, kwenye ndoa, shuleni, na kazini kwa kuzingatia UTU ili apate haki yake kwa wakati hata kwenye ndoa yake.

# SURA YA 1

## Kukata Rufani Kwa Mungu Leo Juu Ya Mateso, Unayopitia Na Mungu Akujibu Leo Kwa Matendo Dhahiri

**Zaburi 77:10** "*Nikasema, ndio udhaifu wangu huo, Lakini nitaikumbuka miaka ya mkono wa kuume wake Aliye juu. Angalia neno hili kinachohitajika ni* ***Imani*** *kwa* ***Mungu tu*** *aliye juu atende muujiza".*

**Matendo ya Mitume 25:11** "*Basi ikiwa ni mkosa au nimetenda neno la kustahili kufa, sikatai kufa; bali, kama si kweli neno hili wanakonishitaki, hapana awezaye kunitia mikononi mwao. Nataka rufani kwa kaisari."*

Hebu angalia neno la Mungu linavyosema, kuwa ikiwa ni *"MKOSA AU NIMETENDA NENO LA KUSTAHILI KUFA SIKATAI"* neno hili linasisistiza ukiwa ni mkosa mbele za haki yaani mbele za MUNGU AU MWANADAMU YEYOTE PASIPO KOSA, HAKUNA WA

KUKUTIA HATIANI, ILA KAMA UNA KOSA TOBA INASTAHILI AU KUFA.

Panahitajika ukweli na haki katika maisha yetu ya kila siku; Kwani usijifiche au usifiche uongo, kwani penye ukweli ama uongo patafichuliwa kwa neema ya Mungu, na malipo yake yapo hapa hapa duniani na sio mahala pengine.

Kwa hiyo mwanadamu yeyote unastahili **TOBA** sahihi, wakati sahihi mbele za Mungu **mfano … (Zab 51:1 Ee "*Mungu, unirehemu, sawasawa na fadhili zako. Kiasi cha wingi wa rehema zako, uyafute makosa yangu. 2 unioshe kabisa na uovu wangu, unitakase dhambi zangu")*.**

Ili uishi na usife bila kukusudiwa kwa makosa bila toba, ama kwa adhabu kabla ya wakati.

Jitahidi utubie dhambi zako kabla rufani haijafuatiliwa kwa mwenye haki mbele za MUNGU, kwani mwenye ukweli mahali popote hapa duniani ni MUNGU tu, na yeye anapokea misamaha yetu yote, na kusahau; Na hapa duniani usishangae wanadamu wanaweza kukufanyia yafuatayo:

# KUKUZULIA UONGO/KUKUSEMEA UONGO

Na ukaoneka ni ukweli kwa watu wengi na watatumia vyombo vya habari ama mitandao kukuchafulia jina au cv yako na utambulisho (identity) wako na walio wengi kwa sababu wanamfuata ibilisi, maana ndiye mwenye nguvu na alitupwa hapa duniani atawale walio wake, ukachafuliwa jina lako baadae uongo wao utachukua nafasi ya kweli, wakaona ni hivo hivo, watasherekea kwa kufanya sherehe, kula vyakula vizuri, na kucheza mziki hadi asubuhi, kwa sababu wameshinda kwa wingi wa uongo juu yako.

**Waraka wa Yakobo 1:12-17 inasema....** ***"Heri mtu astahimiliye majaribu; kwa sababu akiisha kukubaliwa ataipokea taji ya uzima, Bwana aliyowaahidia wampendao. 13 Mtu ajaribiwapo, asiseme, Ninajaribiwa na Mungu; maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu, wala yeye mwenyewe hamjaribu mtu.***

***14 Lakini kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa.***

***15 Halafu ile tamaa ikiisha kuchukua mimba huzaa dhambi, na ile dhambi ikiisha kukomaa huzaa mauti. 16 Ndugu zangu wapenzi, msidanganyike. 17 Kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kwa Baba wa mianga; kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka-geuka.".***

## KUKUCHAFULIA JINA

Hapa ni pamoja na kukuita jina au majina yafuatayo: -

a] Mwizi, b] Mzinzi, c] Mzurumaji, d] Muuaji n.k. Wakati wamepanga njama za kila kitu, kuhusiana na majina haya na ukakamatwa nacho, wakati wanapohitaji kufanya hivyo kwa wakati wanapohitaji mambo yao yakamilike.

Kumbuka wao ni washiriki wakubwa wa dhambi hizi. **Ila wewe nyenyekea kwenye uwepo wa Mungu** naye atakuletea mtu wa kukuinua ama atakuinua kwa wakati wake.

Angali mfano wa ESTHER ALIPOINULIWA NA MFALME KATI YA WANAWAKE ...... **Esta**

**2:15 "*Hata ilipowadia zamu yake Esta, binti Abihaili, mjomba wake Mordekai, ambaye alimtwaa kuwa binti yake, ili aingie kwa mfalme, yeye hakutaka kitu, ila vile vilivyoangizwa na Hegai, msimamizi wake mfalme, mwenye kuwalinda wanawake. Naye huyu Esta alikuwa amepata kibali machoni pa wote waliomwona. 16. Basi Esta alipelekwa kwa mfalme Ahasuero, katika nyumba ya kifalme, mwezi wa kumi ndio mwezi wa saba wa kumiliki kwake".***

Kaa kwenye uwepo wa Mungu, iko siku ya kusafishwa mpendwa mtu wa Mungu**,** usihesabu mabaya mangapi yaliyokutokea kwa wanadamu, kwa Mungu sekunde moja tu ni kicheko cha milele kwa maadui zako.

***"Esta 2:17 Mfalme akampenda Esta kuliko wanawake wote, naye akapata neema na kibali machoni pake kuliko mabikira wote; basi akamtia taji ya kifalme kichwani pake, akamfanya awe malkia badala ya Vashti".***

**AIBU: -H**ii ni pamoja na kukuvua nguo ama kuvalishwa vazi la aibu kwa kunenewa maneno machafu, alimradi wakuondoe kwenye uwepo wa heshima na ukuaji kiroho ama kuongezeka kiuzalishaji.

***"Yakobo 1:19-20...19 Hayo mnajua, ndugu zangu wapenzi. Basi kila mtu na awe mwepesi wa kusikia, bali si mwepesi wa kusema; wala kukasirika; 20 kwa maana hasira ya mwanadamu haiitendi haki ya Mungu."*** Jitahidi usubiri kipindi Mungu alichoweka mbele yako na si kipindi cha mwanadamu, kukusimanga kwa kukuinua**.**

## KUPEWA NAFASI (CHEO):

Jambo hili ni zuri sana, kwani unaweza kuchaguliwa kama kiongozi kwa kupewa cheo, ama kupandishwa cheo kazini ama sehemu yoyote ndani ya familia, kazini, kanisani, kwenye vikundi wakisubiri uongoze vizuri na endapo ukaongoza vizuri ila wapinzani wakiwa wengi ndani ya kundi wanaunda kamati ya chini chini, juu ya nafasi yako kama Yusufu, wanakuja na hoja za kukupinga,

wakiamini wamekumaliza kama Yusufu........Angalia neno linasemaje.

“**Mwanzo 41:*41 Farao akamwambia Yusufu, Tazama, nimekuweka juu ya nchi yote ya Misri..........Hapa Yusufu anainuliwa.42. Farao akavua pete yake ya muhuri mkononi mwake, akatia mkononi mwa Yusufu; akamvika mavazi ya kitani nzuri; na kumtia mkufu wa dhahabu shingoni mwake.44. Farao akamwambia Yusufu, Mimi ni Farao, na bila amri yako, mtu asiinue mkono wala mguu katika nchi yote ya Misri.......ukiendelea mstari wa 45 Yusufu aliozeshwa na binti Asenathi...na 41 Yusufu alibarikiwa wana wawili ukiendelea kusoma*****....”

subiri wakati wako wa kuinuliwa mtu wa Mungu hata kama unakataliwa, au unapitia changamoto za namna gani.

## KUKATALIWA:

Ni jambo la k**awaida kwa watu wenye kibali kwa Mungu** katika dunia ni tendo linalotokea kwenye ngazi ya familia, kazi, ndoa, kanisani ama, au

kikundi chenye mwitikio wa mawazo mazuri yanayofanana ili kuleta mafanikio, na wakatafuta neno ama jambo moja wakaliongezea uchochezi likatengenezwa kuona kuwa wewe ndo umelifanya.

Kwani uko peke yako na huna mtu mwingine mtetezi wako. Jitahidi sana bila shahidi zaidi ya MUNGU UKAE KIMYA NA KUSEMA ***"MTETETEZI WANGU YU HAI" NA "MAPENZI YAKO YATIMIZWE MUNGU".*** Angalia neno hili.

"***Isaya 53:3 Alidharauliwa na watu na kukataliwa na watu; Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, Alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu".*** Ukisoma neno hili limesheheni ujumbe mkubwa sana, kwani hata Yesu alikataliwa na kudharauliwa sana, jifunze kutoka kwa Yesu, jipe moyo na songa mbele Mungu atakuheshimisha siku moja tu.

Kipengele hiki cha ***UBINAFSI*** kinaanzia kwenye ngazi ya **NDOA,** hapa kuna mawifi, shemeji, na wakwe, mara kwa mara kimewagusa na kuwaumiza

watu wengi mpaka kufikia ndoa kunyamaza kimya (**kunyamazishwa /kuvunjika),** pande zote, kwa kumuumiza mtu mmoja aliye kusudiwa, ama kupelekea ndoa kuvunjika kabisa.

Hapa nafasi ya SHETANI anakamata fikra za watu wote na nguvu za mizimu ya familia zinashika kasi, kwani kuna **familia na ukoo** mwingine hauruhusu au haujawahi kupata ndoa, ama mafanikio, ama hawaruhusu watu kuoa na kukaa pamoja, kuzaa, na kuishi kwa furaha na mafanikio, **kunatokea VITA** ya kupelekea watu kutengana, na watu wanaona kawaida yetu sisi hatuolewi hatuoi n.k, kumbe ni **mizimu ya familia**.

Angalia neno hili juu ya **ndoa,** ni eneo ambalo ukisoma **WARUMI 7:1-6** kujua kwa nini mme au mke awe na maamuzi yake pekee ya kuolewa au kuoa. Mwanamme inampasa awe na maamuzi yake peke yake juu ya familia atakavyoiendesha na jinsi ya kuitunza ndoa na familia yake, na ***sio kutegemea marafiki*** na ndugu bali aangalie upande wa pili ili kupata **ushauri** wa ziada kutoka kwa **wazazi,**

**walezi, washauri, wasimamizi wa ndoa, ama wachungaji ambao ni walezi wa kiroho**.

Hili linapelekea muolewaji kuuliwa kwa kupewa sumu ya dawa, kuua uzao ama fikra zake na seli za mwili kwa kupandikiza sumu ya madawa na wakishindwa wanaenda kwenye ushirikina, mitego ya ajali mbali mbali, na wakishindwa yote wanakutenga na kunyamaza kimya. Hakuna anayeongea na wewe familia nzima ya mumeo kwa kuwaambukiza marafiki wa karibu na familia na marafiki wa mumeo.

**Angalia Warumi** ***7: 2-5 “2 Kwa maana mwanamke aliye na mume amefungwa na sheria kwa yule mume wakati anapokuwa yu hai; bali akifa yule mume, amefunguliwa ile sheria ya mume. 3 Basi wakati awapo hai mumewe, kama akiwa na mume mwingine huitwa mzinzi. Ila mumewe akifa, amekuwa huru, hafungwi na sheria hiyo, hata yeye si mzinzi, ajapoolewa na mume mwingine.***

***4 Kadhalika, ndugu zangu, ninyi pia mmeifia torati, kwa njia ya mwili wa Kristo, mpate kuwa mali ya mwingine, yeye aliyefufuka katika wafu, kusudi tumzalie Mungu matunda. 5 Kwa maana tulipokuwa katika hali ya mwili, tamaa za dhambi, zilizokuwako kwa sababu ya torati, zilitenda kazi katika viungo vyetu hata mkaizalia mauti mazao.".***

***Mathayo 5:30-32 "30 Na mkono wako wa kuume ukikukosesha, ukate uutupe mbali nawe; kwa maana yakufaa kiungo chako kimoja kipotee wala mwili wako mzima usitupwe katika jehanum.***
***31 Imenenwa pia, Mtu akimwacha mkewe, na ampe hati ya talaka; 32 lakini mimi nawaambia, Kila mtu amwachaye mkewe, isipokuwa kwa habari ya uasherati, amfanya kuwa mzinzi; na mtu akimwoa yule aliyeachwa, azini."***

Si rahisi kama inavyofikirika kwa mwanadamu wa sasa, kwani matendo hayaendani na Neno la Mungu. Neno limesimama pale pale kuleta habari njema ya watu hawa, kuishi pamoja kwa maridhiano, makubaliano, suluhisho, na pia sio

vyema kutalikiana kama watu wanavyofanya ndoa zao.

Sasa kirahisi na kuwa na mume mwingine, ama mke mwingine, mara baada ya maamuzi ya haraka kwa kuoa tena kwa VYETI vyeti vya ndoa ya madhabahuni, “wanapewa vyeti vya ndoa makanisani, na ndoa zinafungwa na wachungaji, huku na mahakamani wanaenda kutalikiana kwa vyeti pia.

Eneo jingine, ni **kazini**, kwani hapa, watu humuonea wivu mtu mwenye kufanya kazi vizuri, elimu zaidi, ama nidhamu kazini na kumzulia jambo ambalo litamkosanisha na mkuu wa kazi (**boss)** wake, kwa kutumia kashfa ya matendo halisi, ama kumtungia maneno kupitia simu, ya **maandishi**, ama **sauti** (voice record) na hili hupelekea mtu kufukuzwa kazi alimradi wanataka afeli aende mtaani aaibike na asiwe na kazi.

Kama ni mfanyabiashara anazushiwa tendo la kukosa ama kukosana na wateja kwa kauli na matendo ya watu ama, ukorofi na uchonganishi wa

oda mbalimbali zinazotolewa na wateja kukosa kauli nzuri na maneno kugeuzwa mfano kurudisha pesa kwa mteja baada ya kukataa bidhaa, na kurudisha bidhaa zilizokataliwa.

- Eneo hili limegubikwa na

**KUHARIBIKIWA NA KUFIWA KWA VITU** mara, mfano unapopata pesa kutoka kwenye miradi yako mfano shilingi 100,000/- Inatokea hasara ama uharibifu unaohitaji matengenezo ya gharama za laki 300,000/- au zaidi kwa marudio. ***1 Wakorintho 15:53 Maana sharti huu uharibikao uvae kutokufa, nao huu wa kufa uvae kutokufa***.

Mtu wa Mungu Neno la Mungu linasisitiza sana mwanadamu kuvaa kutokufa, yaani maombi yako kwa Mungu yawe ni kuomba uhai na urejesho zaidi ya misiba na kufakufa.

Kwani usipofanya hivyo utakuta, kama una mifugo kama kuku leo ishirini wamekufa kesho 40, mwisho banda linabaki tupu, na magonjwa hakuna, na kama ni nyumbani leo bomba la maji linapasuka, kesho

waya wa umeme unaleta shoti vitu vinaungua, kama ni gesi inamwaga gesi (leakage) alafu mtungi umeununua leo wa kg.15 shilingi 58,000 mfano Oryxy kesho uko wazi kabisaa.

- Na hii haiishii hapo bali hata uzao wako unakuta unapata mimba zinaharibika, kabla ya wakati wa kuzaliwa mtoto, ama mtoto anazaliwa leo na leo leo anakufa kwa sababu zisizo na msingi au mtoto anakufa akiwa mchanga kwenye umri wa miaka 1 hadi mitano kwa sababu za kishirikina.

Hebu tu watu Mungu omba kwa bidii na hasira ili Mungu aione hasira ya maombi yako kwa uaminifu, kutoa sadaka, ili uvuke eneo hili, hata kama ulikabidhiwa umalkia ama uchifu ama ufalme wa mizimu pasipokujua ukuachie kwa jina la Yesu.

***Mathayo 7:8 "Kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye atafunguliwa*. *Mtu wa Mungu"*** Omba mpaka Mungu atakupa majibu yako, usikate tamaa, Elizabeth, Mariam, Sarah, Hana pia waliomba mpaka wakapata baraka ya watoto mfano angalia…***1 Samweli 1:20 "Ikawa, wakati***

***ulipowadia, Hana akachukua mimba na kuzaa mtoto mwanamume; akamwita jina lake Samweli, akisema, kwa kuwa nimemwomba kwa Bwana”***.

## KUKOSA MTU WA KUKUINUA AU KUKUSHIKA MKONO

-Hii ina maana kwamba kila unapoenda ukifika kupokelewa unakuta ukuta ama kizuizi cha kuendelea mbele ili ufanikiwe au upokee majibu yako ya hatma. neno hili likufungue leo.

Angalia ***ISAYA 57:14 “Naye atasema, Tutieni, tutieni, itengenezeni njia, kiondoeni kila kikwazacho katika njia ya watu wangu.*** **Angalia unaishi maisha gani, unaweza kukaribia kupokea Baraka, ghafla inazibwa, ama inatoweka, au mtu anayepaswa kukusaidia unakuta amesafiri siku ya appointment, ama amekufa, ama alihama ile ofisi, na zaidi amegeuza kauli kuwa hawezi kukusaidia leo Unafanyaje? Ni swali lenye kutafakali kwa makini sana na Kumuomba Mungu sana na kuomba akupe msaada zaidi ya huu”.**

# KUKUBALIKA:

Hii ni pamoja na kupendwa na wahusika wanaokuzunguka kwa kukupa ushirika wa kazi, kama ni familia mnaelewana unakuwa mshauri ama msemaji mkuu, kama ni ndoa mwenzi wako anakusikiliza, kama ni kazini unasikilizwa na wafanyakazi, boss anakuita mshauliane jambo la kazi na kama ni kanisani unaitwa utoe nasaha zako juu ya kundi ama kikundi cha kanisani, majirani mnakaa kwa upendo kila unachoongea kinasikilizwa na kinaleta mafanikio kwa wote sio mbinafsi.

Haya yote yanapelekea mwanadamu kukupatia kibali kwenye jamii husika inayokuzunguka, ila si muda mrefu wanakugeuka na kukutengenezea **KASHFA** na kukutenga unakuwa mkiwa kama mtoto yatima asiye na wazai wala ndugu au rafiki......

***Mwanzo 39:21 Lakini" Bwana akakawa pamoja na Yusufu, akamfadhili, akampa kibali machoni pa wakuu wa gereza".*** Ndugu yangu **USIJALI JIPE MOYO**, haya yote ni ya muda yanapita subiri

wakati wa Bwana Mungu anakutengeneza. Ili Yesu aje atende muujiza mpaka washangae. Angalia neno hili......Kitabu cha **Esta 8:1 "*Siku ile mfalme Ahasuero alimpa malkia Esta nyumba yake Hamani, Yule adui ya Wayahudi. Mordekai naye akahudhuria mbele ya mfalme kwa maana Esta alikuwa amedhihirisha alivyomhusu"*.**

## KUTENGENEZEWA MAGONJWA

**1 Wakorintho 15: 26 Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti**. Hili ni jambo ambalo linatengenezwa kiroho baadae kuonekana kimwili. Eneo hili linaanza kama utani mtu akifuatilia na akiuliza kuwa, je unaumwa? ama anauliza kwa kusema naona na ninasikia hauko vizuri sauti yako je unaumwa? Je, umeenda hospitali?

Na, je umepata dawa? na wakati mwingine akikupigia simu, yeye anasisitiza kwa kuuliza hivi "afya yako iko vizuri na ni salama?" baada ya hapo mara kwa mara utatumiwa picha na makala za magonjwa Fulani, na suruhisho la kula vyakula na machapisho ya hospitali, kukutaarifu kuwa hospitali fulani yupo Daktari bingwa juu ya ugonjwa huu. **Yeremia 33:3** anasema niite nami nitaitika,

nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua.

Hivyo kila jambo lina kusudi kwa wakati wake, kama mwamini na mtu wa Mungu kwenda hospitali sio kosa, wala sio dhambi, bali katika kila jambo ufanyalo mtangulize Mungu atangulie kusudi la jambo hilo ili upate msaada wa Mungu kupitia Roho Mtakatifu ndiye mwalimu mzuri atakayekupa mwongozo sahihi ufanye nini. 1 Petro 5:12 kwani ndiyo iwe ndiyo na sio iwe sio, Matendo ya mitume 28:26-31 neno linatuonyesha kuwa kuna watakaoona, lakini hawataamii, na kuna wanatakosikia lakini hawatasadiki, ili kutambua na Mungu akawaponya na matatizo.

Hata hivyo, KWENDA HOSPITALI SIO KUPIGANA KIMWILI bali ni kutafuta suruhisho la kitaalam (kisayansi,) ili upate kujua vipimo vinasemaje na nini kinachokusumbua kwa wakati huo, na ili uanzie wapi kuomba Mungu akuponye na ugonjwa huo, na jinsi ya kutumia dawa utakazopewa na Daktari kwa wakati huo ili dawa hizi zisilete UHATARISHI mwilini mwako bali

zipambane na udhaifu uliojionyesha dhahiri kwenye vipimo, ili kukuweka huru kiafya kutokana na udhaifu ulioonekana., kwani Bwana Yesu Kristo anaponya, kwa imani angalia Luka 15-17, anapouliza .hawakutakasika wote? Wale kenda wako wapi?

Hivyo kutokana na kinga za mwili wa mtu yeyote, kupungua, kutokana na lishe duni, kutokana na hali ya hewa chafu (air pollution), kufanya kazi bila kupumzika (resting), kutokula chakula bora kwa wakati (balance diet), ama udhaifu unaojitokeza mwilini kuchangia kinga za mwili wa mtu kudhoofika ( malnutrition), na hapa unashauriwa usifanye maamuzi yasiyo ya msingi, bali uombe ushauri haraka na uwe na uamuzi wa kwenda hospitali, na hapa usiseme ovyo hali yako kwa watu zaidi ya kwenda magotini kwa Mungu, na kutafuta kwa kina chanzo ama sababisho la tatizo.

Kwani hiyo itakusaidia kutatua vita ya mwilini, hapa dhidi ya vita ya rohoni. Pia kama neno la Mungu linavyosema **2. Kor 10:3** kuwa tunaenenda katika mwili, hatufanyi vita jinsi ya mwili. Na

Warumi 8:37 inayosema “Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda kwa yeye aliyetupenda.

Katika andiko la biblia linatukumbusha jambo kubwa sana kuwa kimya, katika kutimiza kusudi la Mungu, hivyo *sio lazima* uongee mambo yako kwa kila mtu, unaweza kuwa na mtu wa kukushauri hapa kwenye jambo lolote hususani afya yako ili uweze kupata mwongozo, usikae kimya, bali uwe na uchaguzi wa kuwa umwambie nani na wakati gani, na mtu gani jambo lako, ili upate utatuzi wa nini ukifanye kwanza kabla jambo jingine, ukiwa na Roho Mtakatifu akiwa ni mshauri mkuu kwanza na ukasoma neno la Mungu, Kutoka 14:14..” Bwana atawapigania nanyi, mtanyamaza kimya. Na Zab 62:5 Nafsi yangu, umgoje Mungu peke yake kwa kimya. Tumaini langu hutoka kwake.

Bibilia na neno la Mungu inasema magojnwa ni sababisho la uasi na dhambi, **Mathayo 12:43**. Hapa mapepo yanapomtoka mtu hutafuta mahali pachafu ili yaingie. Eneo hili unaweza kutungiwa na kutengenezewa ugonjwa tofauti- ukiwa na hisia

hizo adui anachukua nafasi hiyo kukushambulia, angalia **Yohana 5:14** Yesu anasema usitende dhambi tena. Hapa unaweza kumshinda shetani na adui kwa kutotenda dhambi, ukawa msafi wa Toba ya kweli, ukiomba rehema na matendo yako pamoja na maneno yako yakawa safi ukamshinda adui akashindwa kukushambulia kwa ugonjwa wa aina yoyote aliokusudia,

**Mathayo 17:14** ukiwa mfuasi na mwanafunzi wa Yesu mzuri unashauriwa kufunga na kuomba, Na tofauti na hilo utashambuliwa na adui na atafurahia matokeo yake aliyokusudia mwilini mwako, Hapa kuna mfano halisi wa Kifafa na pumu kwenye biblia (alergy), ni sehemu ya mapepo yanayoandaliwa na mchawi mfano.

Mzuri katika jamii watu wanarusha dawa za aina mbali mbali mfano allergy (kopo), ant malaria, UTI na antibiotic kwa muda mrefu, eneo moja tu la nyumbani na sehemu nyingine unapofanyia kazi kama eneo la biashara na ofisi malangoni kwako, mara kwa mara wakitegemea mtu ataanzia hapo kuumwa ugonjwa huo kwa kusubiri dalili.

Na kweli kifua kitabana sana, kwa waliokuwa wanafanya kazi eneo hili kwa kupiga chafya za uhakika, kutapika na kusikia kizunguzungu ili ukose stamina na uanguke, joto linapanda na dalili zote za kuumwa kwa muda takribani siku kadhaa na, ladha ya chakula mdomoni ikabadilika na kutoweka, kupiga chafya na wao wanachungulia ili kuona kama uko salama, pia wanakuuliza “UNAUMWA?” hii yote inategemea wewe unayo imani na msimamo na Yesu kuwa ndiye mponyaji.

Je? unayo HOFU, WASIWASI NA WOGA NDANI YAKO? NA JE, NI NANI UNAYEMUAMINI AWE MPONYAJI WAKO. Ukimwamini MUNGU, UTAPONA, NA UKIAMINI KALUMANZILA PIA UTAPATA MAJBU YAKE NA MALIPO YAKE.

**Wafilip 2:10-11** kwani inabidi ulimi wako ukiri kuwa YESU ni BWANA na mponyaji. Jambo la kuzingatia, upitapo kwenye njia yenye mitego ya namna hii na majaribu, Tanguliza damu ya Yesu na Jina la Yesu kwa imani kuwa chochote kilichowekwa kwenye malango yoyote, ama njia

kama tego lisikudhuru kwa namna yoyote, bali ukuu wa MUNGU UONEKANE ZAIDI YA UBAYA ULITEGWA, NA USIACHE KUPITA NJIA HIYO KUWAONYESHA, KUWA ULIYEMBEBA NDANI YAKO NI MKUBWA KULIKO MITEGO YAO.

**Yohana 4:4** anaposema kuwa sisi tumetokana na Mungu tumewashinda, kwa sababu yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia, na jaribu kwa mtu ni la wakati tu inalazimu upitie, yaani lazima upitie jaribu ili mapenzi ya Mungu yatimizwe, kwani hicho ni kikombe chako. Kwa wakati huo ili uiendee hatua ya ushindi wa imani kwa Mungu wako.

Ukimuamini Mungu ukaomba na kufunga, utashinda VITA YAO angalia **Wafilipi 4:13** nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu na pale neno la Mungu linavyosema kuwa vita yetu siyo ya damu wala nyama, bali ni ya pepo wabaya **Efeso 6:11-18** na mstari wa **17** anasisistiza ipokeeni chapeo ya wokovu na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu na **2Wakor 4:1-4** Kuwa

ukiwa ndani ya neno la Mungu hutapofuka na kupotea fikra zako kama wasioamini na kukosa nuru ya Kristo Yesu na **2 Kor 10:4** pia hatupashwi kuwa na siraha za vita vya mwili bali zile zenye uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome.

Ushauri wangu hapa simama upigane vita ya kiroho kwa neno la Mungu na maombi utashinda, kulingana na maandiko ya biblia kwa kuvaa dirii ya haki kifuani, kufungiwa miguu utayari, kwa injili ya imani zaidi ukatwae ngao ya imani ambayo itasaidia kuzima mishale yote ya moto wa adui, ipokee na upanga wa roho ambalo ni NENO la MUNGU kwa sala zote na maombi na kukesha ili ushinde.

Usitishike kwani neno la mungu linatushindia **Luka 21:9** anasema mkisikia habari za vita msitishike maana hayo hayana budi kutukia kwanza, lakini ule mwisho hauji upesi kwa maana unaye mtetezi YESU atakushindia vita ya magonjwa yote.

**M**wisho utaona kuwa neno la Mungu linajenga, linatibu, linaokoa, linafurahisha, linaongoza fikra

zako ikiambatanishwa na maombi kama **WAFILIPI 4:4** anasema furahini katika Bwana siku zote, tena nasema furahini.

Zingatia neno la Mungu na utaratibu usitikisike, 1 **Wakorintho 14:40** lakini mambo yote na yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu. Roho za machafuko ni hatari na maendeleo ya kiroho na ya kijamii.

Ni wajibu wa kila mkristo kupambanua kazi ya roho hizi na kuzisimamia kwa mamlaka ya Kristo, tumeitwa kuwa washauri, wapatanishi wa amani si chimbuko la vurugu. Weka mazingira ya maisha yako kuwa safi kiroho, na Mungu wa amani atakutumia kuleta utulivu palipo na machafuko kijamii, kiafya na kiroho.

**HEBU KATAA. KWA JINA LA YESU.**

Hivyo kukata rufani ni kitendo cha kumwambia Mungu kuwa sasa tatizo hili **MUNGU NIMEKUKABIDHI ULIMALIZE BAADA YA KUWA NA UTATA KATIKA UTATUZI**

**NDANI YA UWEZO WANGU, VITA NI YAKO BWANA YESU**, Kama Mtakatifu **RITHA WA** Kashia **ALIVYOKUACHIA NIA YAKE YA KUKUTUMIKIA KAMA MTAWA, NA UKAMJIBU MAOMBI YAKE, SURUHISHO LIKO KWAKO LEO NA LEO UWE MWANZO WA MAFANIKIO KATIKA KUPATA MAJIBU SAHIHI KWAKO BWANA YESU,** haijalishi nimesali wapi, nimeombewa na watu wangapi, SASA **NASEMA BASI KWAKO**, **UWE JIBU KWANGU BWANA YESU.** Nyamazisha kila sauti ndani yangu isiyo na uhalali kutoka kwako Bwana yesu.

SEMA MIMI...................................[***Taja jina lako hapa***] siumwi ugonjwa wowote shetani alionitumia, ama kuutengeneza, ama ugonjwa wa kurithi katika familia au ukoo wetu upande wa mama au upande wa baba, sema sio ugonjwa wangu huu, wala magonjwa haya na ninakiri uponyaji kwa jina la Yesu na kwa damu ya YESU. Sema sitatengwa, sitanyimwa nafasi, haki na kibali, sitasemewa uongo, sitazuliwa mabaya yoyote tena, sitanenewa uongo, sitadharauliwa kwenye jamii.

## KIRI NA USEME HIVI:

**1 Wakorintho 15:25** Maana sharti amiliki yeye, hata awaweke maadui wake chini ya miguu yake.

Bwana Yesu **nimekata rufani kwako**, **nakushukuru umekubali kuwarudisha nyuma, kuwaangusha** na **kunionyesha maadui zangu** wote wanaonifuatilia na kunitesa, **kiroho na kimwili**, ninakuomba leo **uwarudishie mapigigo sawa na vile walivyopanga vije kwang**u **virudi kwao mara saba sabini**.

Kwani wewe Bwana Yesu ni hakimu wa kweli, haupindishi, hauchelewe, wala haukawii ukiweka sahihi na muhuli kwenye nyaraka, ardhi ama andiko na neno lolote, **LAZIMA LITUMIKE, LIJIBIWE SAWASAWA NA ULIVYOKUSUDIA KWA MAADUI ZETU KWA JINA LA YESU.**

- *ASANTE BWANA YESU Kwa kunishindia vita, vifo, mitego, aibu, vikwazo, mauti, iliyopangwa na adui.*

- Asante Yesu kwa kunivua vazi la aibu lililotengenezwa kwa ustadi lakini vazi hilo umenivua na kuwavalisha maadui zangu.

- Asante Yesu Kwa kukomboa hatua zangu zilizo ibiwa.

- Asante Yesu Kwa ufunuo wa yale yaliyo sirini wanayotumia kama vifaa, ndege, wadudu, wanyama na wanadamu kama hila za kuondoa uwepo wako kwangu.

- **Asante Yesu Kwa kurudisha kibali Na nyota, kazi, elimu, huduma, kumiliki kwangu, uchumi wangu, watoto wangu, [mume wangu, / mke wangu] mawasiliano, afya yangu nguo, kampuni, miradi yangu yote na vitu vilivyoibiwa na adui.**

- Asante Yesu kwa kufunga milango yote yaa adui haitafunguliwa tena, na setelaiti zake zote, network yake, screen zote za simu na kompyuta, vyakula vyotevya waziwazi na

ndotoni, mitego ya njiani na mingine hatanipata tena maana umenizingira kwa wigo wako, hawataniaona tena kwa jina la Yesu.

- Nimefunga mlango wa mateso yote leo kwa jina la Yesu, na sasa ninapokea taji ya uuzima, furaha, kicheko, amani, Baraka zote taja (1 mme/mke, watoto, huduma, kumiliki, uchumi, kibali, kampuni, miradi, 2, 4, n.k taja) zilizoibiwa **sasa zimerejeshwa kwa jina na kwa damu ya Yesu Kristo**.

# KUHUSU MWANDISHI

Dorina ni mtoto wa mwisho kwenye familia ya Josiah Kabyemera, alizaliwa Wilaya ya Karagwe Mkoa wa Kagera, kijiji cha Kishao (mtaa Lukajange), alizaliwa mnamo mwaka 1976, na kusoma Shule ya msingi Lukajange, baadae akajiunga Shule ya Sekondari Bugene iliyoko Karagwe, pia akafanikiwa kuhitimu kidato cha nne, na kapata kujiunga na masomo ya kidato cha sita Kiraeni Wilaya ya Rombo, mkoa Kilimanjaro.

Baada ya kuhitimu kidato cha sita alifanikiwa kujiunga na Shahada ya Business Administration in Information Technology (Associate Degree) katika chuo cha Waldorf College Campus ya Dar es Salaam (ambayo Main Campus ni Iowa--Marekani) iliyokuwa chini ya KKKT ambayo sasa ni (DArTU) CHUO KIKUU KISHIRIKI TUMAINI UNIVERSITY. Mwaka 2002.

Baada ya hapo aliweza kuhama toka DArTU na kwenda Kampala International University nchini Uganda nakahitimu mwaka 2005 kozi (Business Administration in Accounts). Pia alifanikiwa

kusoma Uzamili (Maters in International Business Management) mwaka 2007-2009 Nottingham Univeristy Nchini Malaysia ambayo Main Campus ni Uingereza.

Dorina amebahatika kufanya kazi katika kampuni tofauti tofauti mfano, kampuni ya Tiscan na Cotecna, ambazo ni kampui za Waswis na Wafaransa hapa Dar es Salaam-Tanzania 2006 zikijihusisha na Ukaguzi wa mizigo kutoka nje ya nchi (Inspection) kwa njia ya Meli ama Ndege na baadae nilipata fursa ya kujiunga na Benki ya Boroda (Indian Bank –Main branch Dar es salaam) 2007, pia alifanyakazi katika kampuni ya Ujenzi – ukandarasi wa majengo na usanifu majengo Décor Tech (T) Limited kama mhasibu 2009 -2016. Dorina amefunga pingu za Maisha (ndoa) mwaka 2015 akiwa na rafiki yake aliyesoma nae chuo kimoja nchini Uganda Mr. Paul Steven Mpaka. Ndoa hiyo ilifungwa kanisa la Virka Cathedral ya Catholic iliyoko Uganda Fort Portal Dayosisi ya Rwenzori, chini ya uangalizi wa Usharika wa Azania Front alipokuwa msharika kwa baraka na barua ya kuruhusu ndoa nchini Tanzania.

Na sasa Dorina Amejikita sana kwenye kumtumikia Mungu kwa njia ya uimbaji wa Kwaya Kuu KKKT Mapinga, na alijiunga na kundi la Tarumbeta KKKT Mapinga amekuwa kiongozi fellowship, akihubiri neno la Mungu.

Ikiwa ni pamoja na huduma ya maombi na maombezi huku Mungu akifunua karama ya maono mbali mbali, ya Mwalimu wa neno la Mungu amejikita kwenye UTU (HAKI, TOBA, KUOKOA WATU WAPONE, WAWE NA IMANI, AMANI KWENYE NENO LA MUNGU KWA KUPINGA MIZIMU NA MIUNGU YA FAMILIA/UKOO NA UCHAWI KWA KUMFUATA MUNGU PEKEE).

Na akajidhihirisha kwa watumishi na wachungaji juu ya huduma na kuitwa pale anapohitajika kwa njia ya Roho Mtakatifu kuomba, kupitia wachungaji kuomba kuongoza ibada na vipindi vya maombi., na pia kuitwa kwenye huduma ya madhabahuni ili kulisha watu neno makanisa ya Kikristo mfano TAG na Pentekoste, na Makanisa ya kiroho na medhehebu mengine

Baada ya Ndoa Dorina aliamua kujikita kwenye ujasiliamali wa kujiajili eneo la Bunju B kazi ya

STATIONERY inayoitwa D'STAR STATIONERY ambayo alikuwa mbunifu wa nembo iliyo juu ya kitabu hiki 2005 akaanzisha kampuni ya CONSULTATION mara baada ya kumaliza nimepata misukosuko mingi mpaka nimeamua kuandika kitabu hiki, kwani tangu nimezaliwa ni mtu wa kutengwa, kukataliwa, hata masomo yangu yalifanyika kwa shida sana kwa ufadhili wa Kampuni baada ya kuona umahili na uwezo wangu mkubwa hadi kufanya kazi za kiinjinia pasipo kusomea.

(Nimezaliwa kwa makusudi ya Mungu kwani nilitafutwa mtoto wa kike katika watoto nikapatikana hivyo ni nguvu ya Mungu pekee.) Mungu awabariki, karibu sana tuombe pamoja na mnitie moyo na tuombe wote, kazi ya Mungu iendelee. Amina

***Imetayarishwa Na Mwonaji, Mwl.***

***Na Mtumishi Dorina***
***© 2025***
***YESU ASANTE***